SINCE 1922

eabl

CELEBRATING LIFE




# 2022 INTEGRATED REPORT & FINANCIAL STATEMENTS

# Taarifa ya Mwenyekiti wa Kundi

## Ripoti ya Mwaka wa Kifedha wa 22 Kwa Ufupi

Katika mwaka wa kifedha wa 22, katika East African Breweries PLC (EABL) tulishuhudia mataifa ya kanda hii yakijikwamua kiuchumi kutoka kwa athari za janga la Covid 19. Kama mjuavyo, miaka miwili ya kifedha iliyopita kwetu iliathiriwa sana na janga hilo, na kipaumbele chetu kimekuwa ni kuwakinga watu na biashara yetu. Mwaka wa kifedha wa 22 umekuwa mwema: sio tu kwamba tumeshuhudia mataifa Afrika Mashariki yakifungulia tena shughuli za kiuchumi, bali pia tumeona biashara yetu ikirejelea kawaida.

Licha ya changamoto zilizokuwepo, kuwa na mwelekeo pamoja wepesi wa kubadilika vilituwezesha kupitia changamoto zilizokuwepo na kumaliza mwaka tukiwa imara zaidi, na kutuwezesha wka mara nyingine kuandikisha matokeo mazuri ya kifedha. Kiwango chetu cha wafanyakazi wetu kushiriki kimeendelea kuwa cha juu na tunaendelea kuwekeza kwa ajili ya ukuaji wa kipindi kirefu, katika nembo zetu na bidhaa zetu. Kama biashara inayoongozwa na wateja, huwa twachukua muda kudadisi soko na kuyaelewa vyema mahitaji na matamanio ya mteja na njia gani bora ya kukidhi mahitaji hayo. Hii ndiyo sababu tumeendelea kuwekeza katika uvumbuzi na ubunifu kuboresha bidhaa zetu ili kuendana na mitindo ya wateja inayobadilika.

Bodi na wasimamizi wamejitolea kutoa thamani ya kipindi kirefu kwa wadau wetu. Tunaposherehekea miaka 100 ya shughuli za EABL, tutaendelea kujizatiti kuwa kampuni yenye matokeo bora zaidi, ya kuaminika zaidi na inayoheshimiwa zaidi Afrika.

## Mazingira ya Uendeshaji Shughuli katika Kanda

Mwaka wa kifedha wa 22 serikali za mataifa ya Afrika Mashariki zilipiga hatua kubwa katika utoaji wa chanjo dhidi ya Covid 19 na kuchangia kuondolewa kwa vikwazo vilivyokuwa vimewekwa kuhusiana na janga hilo kwa sehemu kubwa ya mwaka huo wa kifedha.

Hatua hiyo ilichangia kuimarika kwa mazingira ya uendeshaji shughuli kwani vituo vingi vilifungua tena biashara na shughuli za watumiaji wa bidhaa zetu zikaongezeka. Kama Kundi, tunaendelea kuwa moja ya wanaochangia pakubwa katika mapato ya serikali katika kanda, ambapo huwa tulilipa kodi ya Kes 87.7 bilioni mwaka huo.

Kanda ya Afrika Mashariki ina baadhi ya viwango vya juu zaidi vya ushuru wa bidhaa Afrika kusini mwa



> **Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi, ningependa kuwatambua na kuwashukuru wateja wetu, wanaotumia bidhaa zetu, wasambazaji wetu, washirika, na mamlaka pamoja na serikali katika mataifa husika tunayohudumu kwa ushirikiano wao na kwa kutuunga mkono.**

Sahara. Mfumo wa ushuru huo Kenya umeendelea kuwa mkali na usiotabirika, jambo linalozua wasiwasi kwa biashara kama yetu. Tumeendelea kueleza wasiwasi wetu kwa wadau husika kuhusu umuhimu wa nyongeza ya ushuru ya maana ili kulinda maslahi ya watumiaji wa bidhaa na serikali, pamoja na mapato ya sekta hii.

Kama biashara, tuliweza kuhimili ongezeko la mfumko wa bei na kuongezwa kwa ushuru wa bidhaa kupitia kuongeza bei ya bidhaa zetu kwa busara na pia kudhibiti gharama na hili likatuwezesha kupata faida yetu ya juu zaidi katika kipindi cha miaka 5.

Ni katika mazingira haya ambapo mgawo wa faida wa muda wa Kes 3.75 kwa kila hisa ulilipwa mapema mwaka huo. Bodi ya Wakurugenzi imependekeza pia mgawo wa mwisho wa faida wa Kes7.25 kwa kila hisa ulipwe mnamo au kabla ya 30 Oktoba 2022 kwa wenyehisa ambao watakuwa kwenye sajili wakati wa kufungwa kwa biashara mnamo 15 Septemba 2022, baada ya kutozwa kodi ya zuio. Hii pamoja na mgawo wa faida wa muda imefanya mgawo wa faida kwa jumla mwaka huo kuwa Kes11.00 kwa kila hisa.

## Kusaidia jamii yetu

Katika mwaka huo, tuliisaidia sekta ya hoteli na baa kupitia mkakati wa thamani ya US$5 milioni kwa jina Raising the Bar. Fedha hizo ziliwezesha kutolewa kwa usaidizi wa vitu mbalimbali na wa kidijitali kwa baa zilizokuwa zinawakaribisha tena wateja baada ya kufungwa kwa muda mrefu. Tulisaidia pia juhudi za serikali za Afrika Mashariki katika mipango ya kukabiliana na Covid 19, kutoa chanjo kwa wafanyakazi wetu, familia zao, na watumiaji wa bidhaa zetu.

Kujitolea kwetu kuhamasisha unywaji pombe kwa busara ni nguzo kuu katika biashara yetu. Tunataka kubadilisha jinsi wateja wetu wanavyokunywa pombe. Hii ina maana ya kuhamasisha kunywa kwa wastani na pia kuendelea kuangazia madhara ya pombe kwa kubadilisha mitazamo. Pia, kupanua miradi yetu inayoangazia kukabiliana na unywaji pombe kwa watu wasiotimiza umri ulioruhusiwa, kuendesha magari watu wakiwa walevi na pia ulevi wa kupindukia. Kuhamasisha unywaji pombe kwa kipimo na kuangazia madhara ya pombe sio tu kwamba ni jambo njema la kufanya, bali pia ni sehemu kuu ya azma yetu.

Kama biashara, mafanikio yetu ya kifedha yanategemea sisi kuwa na manufaa kwa jamii, maeneo tunamoishi, kufanyia kazi, kununua bidhaa na kuuza. Tunataka wateja wetu wanywe kwa njia bora zaidi, si kwamba eti wanywe zaidi – na wapande na kunywa vinywaji vyetu vya ubora wa hali ya juu na ladha bora zaidi.

Tumeendelea pia kujibu mahitaji ya wateja wetu na bidhaa zetu zina madhara ya chini sana kwa mazingira. Kama biashara, tumechukua mwelekeo wa kimkakati katika ajenda yetu ya Mazingira, Jamii na Utawala (ESG) ambayo huangazia Spirit of Progress, ambao ni mpango wetu wa uendelevu wa miaka 10. Mpango huu una ajenda tatu ambazo ni kuhamasisha mazuri, kutetea thamani ya tofauti zetu na kujumuisha wote na pia kuhakikisha uendelevu kuanzia kwa nafaka hadi kwenye chupa katika mfumo wetu wa uzalishaji.

> **Kujitolea kwetu kuhamasisha unywaji pombe kwa busara ni nguzo kuu katika biashara yetu. Tunataka kubadilisha jinsi wateja wetu wanavyokunywa pombe. Hii ina maana ya kuhamasisha kunywa kwa wastani na pia kuendelea kuangazia madhara ya pombe kwa kubadilisha mitazamo. Pia, kupanua miradi yetu inayoangazia kukabiliana na unywaji pombe kwa watu wasiotimiza umri ulioruhusiwa, kuendesha magari watu wakiwa walevi na pia ulevi wa kupindukia.**

## Kutazama Mbele

Kama biashara, tunaingia kwenye siku za usoni tukiwa na urathi na msingi tulioujenga kwa miaka 100 iliyopita. Ahadi yetu inasalia kuwa kukuza biashara yetu kwa njia imara na endelevu. Tuna imani katika mkakati wetu wa kipindi kirefu, nguvu ya nembo zetu na sifa za kipekee na vipaji vya wafanyakazi wetu. Tukiwa na haya yote, tupo katika nafasi nzuri ya kukabiliana na changamoto na kutumia vyema fursa na hivyo kuendelea kupata ukuaji endelevu kote Afrika Mashariki, na pia kutimiza lengo letu kuu ya kusherehekea maisha kila siku, pahala popote.

## Shukrani

Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi, ningependa kuwatambua na kuwashukuru wateja wetu, wanaotumia bidhaa zetu, wasambazaji wetu, washirika, na mamlaka pamoja na serikali katika mataifa husika tunayohudumu kwa ushirikiano wao na kwa kutuunga mkono.

Ningependa pia kuwatambua na kuwashukuru Wasimamizi wetu na wafanyakazi wetu kwa kuendelea kuwa wepesi wa kuchukua hatua na kufanya kazi katika mwaka huo wote. Wamedhihirisha kujitolea sana katika biashara yetu. Kadhalika, wepesi wa kubadilika kipindi cha kutotabirika, na ubunifu na uvumbuzi wao ambavyo vimewezesha biashara yetu kubadilika kuendana na hali na pia kujifunza mengi kutokana na kipindi hicho cha janga.

Vilevile, ningependa kuwashukuru wanachama wenzangu kwenye Bodi na wanachama wa bodi za kampuni zetu tanzu kwa ushauri wao, uungaji mkono na kujitolea kwao mwaka huo wote na pia kwa kuwezesha mazingira mazuri na imara ya utawala wa kampuni.

Sina shaka kwamba tutatokea imara zaidi na wenye imani ya kutumainia siku za usoni za ufanisi.

**Dkt. Martin Oduor-Otieno**
**Mwenyekiti wa Kundi**